HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE
IDARA YA ELIMU SEKONDARI

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI-MACHI 2021.

1.0: UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ina jumla ya Shule **5** za sekondari zenye jumla ya wanafunzi **2017** kati ya hao wavulana ni **989** na wasichana ni **1028** ambazo ni Inyonga, Utende,Ilunde,Isack Kamwelwe na Ilela zenye usajili wa kudumu na zinazomilikiwa na Serikali. Shule zote hupokea wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne, isipokuwa kwa shule moja tu ya Inyonga ambayo inapokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita kwa wavulana na wasichana kuanzia Julai **2016.**

2.0: SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA IDARA MWEZI JANUARI-MACHI, 2021.

1. Kuratibu na kusimamia masuala ya taaluma katika shule za sekondari.
2. Kusimamia ujenzi wa miundombinu katika shule za Sekondari Ilela,Utende,Isack Kamwelwe,Ilunde,Kamsisi na Kamalampaka.
3. Kushughulikia urekebishaji wa takwimu za wanafunzi katika mfumo wa PREMS
4. Kusimamia na kuratibu kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021.
5. Kusimamia na kuratibu utengenezaji wa madawati ya wanafunzi wa shule za sekondari.
6. Kuratibu na Kusimamia zoezi la kuendelea kuchukua tahadhali ya magonjwa ya mlipuko hasa ugonjwa wa Covid 19.
7. Kusimamia ufanyikaji wa mtihani wa pamoja wa robo muhula wa shule za Sekondari kidato cha I, II, III na cha IV 2021.
8. Kusimamia umaliziaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara za masomo ya sayansi katika shule za sekondari Ilunde,Isack Kamwelwe,Kamsisi na Kamalampaka.
9. Kusimamia ufanyikaji wa mtihani wa utamilifu Mkoa wa kidato cha sita 2021.
10. Kusimamia na kushiriki katika zoezi la kufanya tathimini ya matokeo ya darasa la saba ya mwaka 2020 Mkoani.
11. Kupokea na kufanya tathimini ya matokeo ya upimaji kitaifa kidato cha pili na matokeo ya mtihani wa Taifa kidato cha nne 2020.
12. Kufuatilia zoezi la ufunguaji shule za Sekondari kwa muhula wa kwanza 2021.
13. Kuratibu na kushughulikia maandalizi ya UMISSETA mwaka 2021.

Na	LENGO	SHUGHULI	UTEKELEZAJI
1.	Kuratibu na kusimamia masuala ya taaluma katika shule za sekondari	Kusambaza fomu za ufundishaji shuleni kupitia kwa waratibu wa elimu kata.	Shule zote tano zimejaza fomu za ufundishaji kupitia kwa Waratibu Elimu Kata(MEK) na kuwasilisha ngazi ya Halmashauri kwa ufuatiliaji zaidi.
2.	Kusimamia ujenzi wa miundombinu ya Shule.	Shule ya sekondari Ilela imepokea fedha kutoka Ep4r Tsh. **40,000,000**, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na Utende Tsh. **40,600,000**, Kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na matundu sita (6) ya vyoo.	Shule ya Sekondari Ilela ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa ujenzi umekamilika na Shule ya Sekondari Utende ujenzi wa vyumba viwili (2) vya madarasa na matundu sita (6) ya vyoo ujenzi umekamilika.
3.	Kuratibu na kusimamia ufanyikaji wa tathimini ya matokeo ya mtihani wa kidato cha pili na cha nne	Idara imeshiriki kikamilifu kuhakikisha tathimini ya matokeo ya upimaji kidato cha pili 2020 na mtihani wa taifa kidato cha nne 2020 unafanyika.	Jumla ya wanafunzi **430**, wavulana **216** na wasichana **214** walifanya mtihani wa upimaji kidato cha pili 2020, waliofaulu wavulana **216** wasichana **214** jumla **430** ikiwa ni sawa na asilimia **90.00** ya ufaulu. kidato cha nne

	2020 unafanyika.		waliofanya mtihani wa taifa jumla ni **253** wavulana **129**,wasichana **124**,waliofaulu wavulana **129**,wasichana **121** sawa na asilimia **98.81** ya ufaulu na waliofeli wavulana **0** wasichana **0** sawa na asilimia **1.19**.
4.	Kushughulikia urekebishaji wa takwimu za wanafunzi katika mfumo wa PREMS	Idara ya Elimu sekondari ilishughulikia takwimu za wanafunzi katika nyanja za ubadilishaji shule,uhamisho na usajili wa wanafunzi katika mfumo wa takwimu za wanafunzi wa sekondari (PREMS).	Wanafunzi **06** (Wav **03 na** Was **03)** wamehamishwa/wamebadilishiwa shule kulingana na maombi ya wazazi wao.
5.	Kuratibu na kusimamia ufanyikaji wa mtihani wa utamilifu wa kidato cha sita Mkoa 2021	Idara imeshiriki kikamilifu kuhakikisha mtihani wa utamilifu kidato cha sita 2021, Mkoa unafanyika kama ulivyopangwa.	Jumla ya wanafunzi **146**, wavulana **70** na wasichana **76, wamesajiliwa** waliofanya mtihani wa utamilifu kidato cha sita Mkoa 2021, ni wanafunzi **144.**
6.	Kusimamia na kuratibu matarajio ya uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza **2020/2021**.	Kuingiza kwenye mfumo (Selection MIS) majarajio ya wanafunzi watakaojiunga kidato cha kwanza kwa kila shule **2020/2021**.	Idadi ya wanafunzi watarajiwa **687** wameingizwa kwenye mfumo wa **Selection MIS.**
7.	Kusimamia uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021.	Idara ya Elimu sekondari ilishiriki kwenye zoezi la kuchagua wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza 2021.	Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza ni **635** wavulana **326** na wasichana **309**.Walioripoti mpaka kufikia tarehe 23/03/2021 ni wavulana **323** wasichana **306** na kufanya jumla **629** ni asilimia **99** ya uripoti.Wanafunzi wasioripoti ni

			6.
8.	Kuratibu na kusimamia ufanyikaji wa mtihani wa pamoja wa robo muhula kwa shule za sekondari kidato cha I, II, III na IV 2021.	Idara imeshiriki kikamilifu kuhakikisha mtihani wa pamoja wa robo muhula unafanyika.	Wanafunzi wa kidato cha kwanza,pili,tatu na nne walifanya mtihani wa pamoja wa robo muhula kwa shule zote za Sekondari ambazo ni Inyonga,Ilela,Ilunde,Isack Kamwelwe na Utende
9.	Kushiriki kwenye kikao cha tathimini ya matokeo ya darasa la saba **2020.**	Idara ya elimu sekondari ilishiriki kwenye kikao kilichoitishwa mkoani katika ukumbi wa idara ya maji.	Tathimini ya matokeo ya darasa la saba ilifanywa Mkoani tarehe **08/01/2021** na kuweka mikakati na maazimio ya pamoja ili kuongeza ufaulu kwa mwaka **2021**.
10.	Kuratibu na Kusimamia utoaji wa tahadhari ya magonjwa ya mlipuko hasa **Covid 19**.	Idara ya elimu sekondari imewaandikia barua wakuu wa shule zote tano za sekondari kuendelea kuchukua tahadhari za ugonjwa wa **covid 19**	Shule zote tano (**05**) za Halmashauri ambazo ni Inyonga,Ilela,Isack Kamwelwe,Ilunde na Utende zinaendelea kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya juu ya kujikinga na kuchukua tahadhari za Magonjwa ya mlipuko ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa **Covid 19** kwa kuwaelekeza wanafunzi,walimu na watumishi wengine wote wa shule kwa kunawa Maji tiririka na sabuni,uvaaji wa Barakoa,kuepuka misongamano nk.

11.	Kupokea fedha za umaliziaji wa vyumba vya maabara za masomo ya sayansi kwa shule za sekondari **Tsh. 180,000,000.**	Kumalizia ujenzi wa vyumba vya maabara za masomo ya sayansi kwa shule za sekondari 2021.	Shule za sekondari zimepokea fedha za umaliziaji wa vyumba vya maabara za masomo ya Sayansi kutoka Serikali kuu,Shule hizo ni Ilunde Sekondari,Isack Kamwelwe Sekonadari na shule mpya tarajiwa za Sekondari za Kamsisi na Kamalampaka.Taratibu za kuanza umaliziaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara unaanza mara moja kama maelekezo ya Serikali yanavyosema.Matangazo ya tenda za wazabuni yamesha bandikwa kwenye Mbao za matangazo.
12.	Kuanza ukataji wa Magogo kwa ajili ya utengenezaji wa Madawati ya shule za Sekondari.	Shughuli ya ukataji wa magogo inatarajia kuanza hivi karibuni.	Utaratibu wa maandalizi ya ukataji wa Magogo umeshakamilika ili zoezi la ukataji wa Magogo lianze kwa ajili ya kuchana Mbao za kutengenezea Madawati,kibali kutoka (Wakala wa Misitu Tanazania) **TFS** ndicho kinasubiliwa.
13.	Kusimamia ujazaji wa fomu za selform za wanafunzi wa kidato cha nne **2020**.	Idara ya elimu sekondari imeshirikiana na wakuu wa shule kuhakikisha selform zinajazwa kwa umakini na kwa wakati uliopangwa.	Ujazaji wa selform umekamilika kwa shule zote tatu ambazo ni Inyonga,Ilela na Utende,zimejazwa kwa umakini na kukamilika kwa wakati.

3.0: CHANGAMOTO

Katika kutekeleza majukumu yake, Idara inakabiliana na changamoto zifuatazo: -

1. Shule zote za sekondari kuwa na walimu wachache wa masomo ya sayansi kulinganisha na masomo ya Sanaa, mahitaji ya walimu wa Sayansi ni 27 na waliopo ni 20 ukilinganisha na mahitaji ya walimu wa Sanaa 32 na waliopo ni 48.

2. Utoro wa rejareja unachangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi.

3. Upungufu wa walimu wa kike shuleni kwa shule zenye Hosteli hivyo kufanya huduma za wanafunzi wa kike waishio hosteli kuwa ngumu kwa kuzingatia jinsi yao, walimu wa kike ni **12** tu kati ya walimu **74** waliopo.

3.1: UTATUZI WA CHANGAMOTO

1. Kuomba Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuongeza idadi ya walimu wa masomo sayansi na walimu wa kike.

2. Wakuu wa shule, bodi za shule na wazazi kushirikiana katika kuendelea kudhibiti tatizo la utoro wa wanafunzi shuleni.

Naomba kuwasilisha,

Timothy E.Bernard

Afisa Elimu Sekondari

HALMASHAURI YA WILAYA MLELE.